



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

IDARA YA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA

TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutangazia Umma na Wananchi wote kwa ujumla kwamba ni marufuku kwa magari yanayopita nchini kueleka nchi jirani yaani (IT- In Transit) pamoja na magari yanayobeba mizigo inayopita nchini kuelekea nchi jirani (Mizigo ya Transit) kuegeshwa katika vituo vya mafuta (Fuel Filing Station) au sehemu yoyote ambayo haijaidhinishwa au kupata ruhusa husika kutoka kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa.

Aidha Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwakumbusha Madereva, Wasafirishaji na Mawakala wa Forodha kufuata **Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka, 2004** pamoja na **Kanuni zake za Mwaka 2010**. Kinyume na hapo adhabu kali itatolewa kwa watakaokiuka agizo hili.

“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”

J. S. Nyomolelo

Kny: **Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa**